

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



Simu: +255734047775
Barua pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz



Kilimani,
Mtaa wa Nyerere,
S.L.P. 1049,
DODOMA.

Tamko la THBUB katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu - Disemba 3, 2024

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wote wa kimataifa, kikanda na kitaifa katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu (International Disability Day).'

Siku hii ya kimataifa ya watu wenye ulemavu, ni matokeo ya Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Na. 47/3, 1992 ambapo ilipitishwa kuwa Disemba 3 ya kila mwaka ni Siku ya Maadhimisho ya Watu wenye Ulemavu Duniani. Maadhimisho haya yamelenga kuhamasisha jamii kutambua haki na fursa sawa na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika masuala ya maendeleo, mahitaji yao, changamoto zinazowakabili na kutafuta namna ya kukabiliana nazo.

Maadhimisho ya mwaka huu, yanafanyika kitaifa Jijini Dar es Salaam na yanaongozwa na kauli mbiu isemayo: "***Kukuza uongozi wa watu wenye ulemavu kwa ajili ya Mustakabali jumuishi na endelevu***" Kauli mbiu hii inaikumbusha Serikali kuona umuhimu wa kuongeza jitihada za dhati kwa

kutoa fursa za uongozi kwa watu wenye ulemavu ili waweze kushiriki na kuongoza kikamilifu shughuli mbalimbali zikiwemo za Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii.

THBUB inatambua jitihada mbalimbali zilizofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kulinda na kutetea haki za Watu wenye Ulemavu nchini ikiwa ni pamoja na: kuwateua watu wenye ulemavu kushika nafasi mbalimbali za uongozi; kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu kwa kufanya maboresho katika ujenzi wa majengo mapya ya umma ambayo yanajengwa kwa kuzingatia ufikikaji (accessible buildings) kwa makundi ya Watu wenye Ulemavu; kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya Watu wenye Ulemavu; na kutoa vipaumbele vya ajira na mikopo ya elimu ya juu. Aidha, Serikali imeendelea kukemea na kuchukua hatua kwa mtu au watu wanaobainika kufanya vitendo vya ukatili, mauji, ubaguzi, unyanyasaji na unyanyapaa dhidi Watu wenye Ulemavu.

THBUB inaipongeza Serikali kwa kuonesha jitihada za kulinda na kutetea haki za Watu wenye Ulemavu.

THBUB inatoa rai kwa umma, kutowaficha watu wenye ulemavu kwa kuwa pamoja na hali yao, bado ni binadamu na wanastahili kutambuliwa bila ya kujali hali yao ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa mamlaka za Serikali zilizopo kwenye maeneo wanayoishi juu ya vitendo vya ukatili, ubaguzi, udhalilishaji, unyanyasaji, unyanyapaaaji kwa watu wenye ulemavu. Pia, wito unatolewa kwa wananchi kuachana na imani, mila, desturi na mitazamo potofu ambayo huwafanya watu wenye ulemavu kujiona

hawakubaliki, hawawezi na hawana mchango kwa jamii inayowazunguka na Taifa kwa ujumla katika shughuli zinazohusu maendeleo.

THBUB inawaomba wadau wote kuungana pamoja kutoa elimu kwa jamii kupinga vitendo vyote vya ukiukaji wa haki za Watu wenye Ulemavu na kuwahamasisha kushiriki kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mwisho, THBUB itaendelea kushirikiana na Watu wenye Ulelemvu na wadau wote wa utetezi wa haki za binadamu katika kuhakikisha kuwa haki zao zinalindwa.

Imetolewa na:



Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mstaafu) Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Disemba 3, 2024